HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

MASHARTI YA KUPATA LESENI

LESENI YA BIASHARA

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya biashara ili mradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18), awe mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai na awe na eneo la kufanyia biashara linalokubalika kisheria.

UTARATIBU WA KUPATA LESENI YA BIASHARA

Mwombaji anapaswa kujaza fomu ya maombi ya leseni (TFN 211) kikamilifu na kuambatanisha kivuli cha:-

i. Jina la Biashara kama sio mtu binafsi (Certificate of Incorporation).

ii. "Memorandum and Articles of Association" kama ni Kampuni".

iii. Kitambilisho cha Uraia, Kitambulisho cha mpiga kura, Leseni ya udereva, Cheti cha kuzaliwa au Hati ya kiapo kuonyesha kuwa ni Mtanzania na kwa mgeni (ambaye sio raia) Hati ya kuishi nchini daraja la "A" (Residence Permit Class "A").

iv. Hati ya ki-Uwakili (Power of Arttoney) kama wenye hisa wote wapo nje ya Nchi.

v. Hati ya kujiandikisha kama mlipa kodi (Tax identification Number-TIN).

vi. Hati ya malipo ya kodi kwa kipindi husika (Tax clearance certificate).

Kwa leseni zinazodhibitiwa na Mamlaka mbalimbali, (Mfano- TFDA, EWURA, CRB nk.) mwombaji lazima kuwa na leseni ya Mamlaka husika kabla ya kuomba leseni ya biashara.

Baada ya kujaza fomu ya maombi ya leseni na kukamilisha viambatanisho, maombi hupitiwa na ngazi zote zinazotakiwa kisheria –Mipango Miji na Afya. Baada ya hapo leseni hutolewa ndani ya siku mbili au tatu.

MASHARTI YA LESENI

1. Mwenye leseni hataweka masharti yoyote kwa mnunuzi.

2. Mwenye leseni atatoa risiti kwa mauzo yote.

3. Mwenye leseni hatatoa huduma/hatauza bidhaa ambazo hazizingatii viwango vya ubora viliowekwa na vyombo vinavyohusika kisheria.

4. Mwenye leseni anaweza kunyang'anywa wakati wowote ikiwa itaonekana aliipata kwa njia ya udanganyifu au amekiuka masharti ya leseni.

MAKOSA

i. Kuendesha biashara bila leseni.

ii. Kuendesha biashara eneo tofauti na linaloonyeshwa kwenye leseni.

iii. Kutumia leseni moja kufanyia biashara zaidi ya moja au maeneo mawili tofauti.

iv. Kushindwa kuonyesha leseni ya biashara inapotakiwa kufanya hivyo na Afisa aliyeidhinishwa na Serikali.

v. Kutokuweka leseni ya biashara mahali ambapo inaonekana kwa urahisi.

vi. Kutoa maelezo ya uongo ili kupata leseni au kukwepa ada/kodi inayostahili.

vii. Kumzuia Afisa aliyepewa mamlaka ya kukagua kufanya kazi yake.

Mtu yeyote anayetenda mojawapo ya makosa hapo juu adhabu yake ni faini isiyopungua Tshs 50,000/= na isiyozidi Tshs. 100,000/= au kifungo kisichozidi miaka miwili (2) au kifungo na faini kwa pamoja.

LESENI ZA VILEO

Sheria ya leseni za Vileo imenyumbulisha aina mbalimbali za leseni za vileo zinazoweza kutolewa chini ya sheri hii:

1. **Retailers On Licence:**
   Leseni hii inamruhusu wenye biashara kuuza pombe na kunywa eneo la biashara.

2. **Retailers Off Licence:**
   Leseni hii haimruhusu mtu kunywea pombe eneo la biashara bali mtu kununua na kwenda kunywea majumbani (Take away) kama grcery.

3. **Wholesale Licence:**
   Leseni hii ni kuuza pombe jumla

4. **Hotel Licence:**
   Leseni hii humruhusu mwenye leseni kuuza pombe kwa ajili ya kunywea katika eneo la biashara kwa watu waliopanga hotelini kwa wakati wowote wa mchana na usiku.

5. **Restaurant licence:**
   Leseni hii inamruhusu mwenye leseni kuuza pombe kwa mtu yeyote anayekula chakula katika mgahawa katika muda was aa 6.00 mchana hadi saa 8.00 mchana na saa 12.00 jioni hadi saa 6.00 usiku.

6. **Members Club Licence:**
   Leseni hii huruhusu uuzaji wa pombe kwa kiasi chochote kwa mwanachama wa Klabu na wageni wao tu.

TEMPORARY LICENCE

Leseni hii humruhusu mtu mwenye leseni kuuza pombe katika sehemu iliyotajwa kwenye leseni mahali penye burudani, starehe au mkusanyiko mwingine kwa kipindi kisichozidi siku tatu.

LOCAL LIQUOR LICENCE – (POMBE ZA ASILI)

Class A Local Liquor:

Leseni hii humrusu mwenye leseni kutengeneza pombe za asili (kienyeji) katika sehemu iliyotajwa na kuuza kwa ajili ya kunywea sehemu ya biashara au nje ya sehemu ya biashara.

Class B Local Liquor:

Leseni hii humruhusu kutengeneza pombe za asili sehemu iliyotajwa na kwenda kuuzia sehemu nyingine iliyo na leseni ya kuuza pombe za asili.

Class C Local Liqour:

Leseni hii humruhusu kutengeneza pombe za asili katika sehemu iliyotajwa kwenye leseni na kuuza kwa mwenye leseni Class D au Class E.

Class D Local Liquor:

Leseni hii humruhusu kuuza pombe za asili katika sehemu iliyotajwa kwenye leseni na kunywea eneo la biashara.

Class E Local Liquor:

Leseni hii humruhusu kuuza pombe za asili kwa ajili ya kunywea sehemu nyingine mbali na eneo la biashara.

MASHARTI YA KUPATA LESENI

Mtu yeyote raia wa Tanzania anayo haki ya kupatiwa leseni ya Vileo ilimradi awe ametimiza umri wa miaka kumi na nane (18), mwenye akili timamu ambaye hajawahi kupatikana na kosa la jinai na awe na eneo la kufanyia biashara linalokubalika kisheria.

UTARATIBU WA KUPATA LESENI

i. Mwombaji hujaza fomu za maombi zinazotolewa na Halmashauri ya Wilaya.
ii. Eneo/jengo linalokusudiwa kufanyia biashara hiyo kukaguliwa na Afisa Afya, Afisa Mipango Miji, Polisi, Afisa Mtendaji wa Kijiji na Afisa Biashara wa Halmashauri na hutoa maoni yao kwenye fomu husika.
iii. Maombi hayo hupelekwa katika Mamlaka ya Utoaji wa Leseni za Vileo ya Halmashauri ya Wilaya kwa uamuzi
iv. Mwombaji ambaye maombi yake yamepitishwa hupewa leseni baada ya kulipa ada inayotakiwa na ni lazima awe amekamilisha masharti ya kupata leseni hapo juu.

VIWANGO VYA ADA

Viwango vya ada vinavyotumika kwa sasa kwa aina mbalimbali za leseni na kama zifuatavyo:-

1. Retailers On Licence (Baa) - 30,000 hadi 40,000
2. Retailers Off Licence (Grocery) - 20,000 hadi 30,000
3. Wholesale (Jumla) - 10,000 hadi 20,000
4. Members Club Licence (Klabu wanachama) - 10,000 hadi 20,000
5. Restaurant & Retailers On Licence - 30,000 hadi 40,000
6. Temporary Licence (Leseni ya muda) - 7,000 hadi 15,000
7. Hotel Licence (Leseni ya hoteli) - 30,000 hadi 40,000
8. Retailers Off Licence non-spirituous - 10,000 hadi 15,000
9. Retailers On Licence non-spirituous (Stores) - 10,000 hadi 15,000

- Mamlaka ya Vileo itaamua kiwango cha ada kitakachotozwa kati ya kiwango cha chini na kile cha kima cha juu. Viwango vinavyotumika kwa sasa na Halmashauri ya Wilaya ni vile vya kima cha juu kwa kila aina ya leseni.

MASHARTI YA UTUMIAJI

Leseni za vileo zina masharti mengi ikiwa ni pamoja na kutouza kilevi kwa watoto . Masharti mengine ni muda wa kuuza pombe na kelele za muziki.

MUDA WA KUUZA POMBE

BAA (Retailers On licence)

(a) Maeneo ya mjini:

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 12.00 jioni hadi saa 5.00 usiku.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 5.00 asubuhi hadi saa 6.00 usiku.

(b) Maeneo ya vijijini:

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 9.00 alasiri hadi saa 2.00 usiku.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 8.00 mchana hadi saa 5.00 usiku.

GROCERY (Retailers Off Licence)

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 2.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 3.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni.

POMBE ZA ASILI (Local Liquour Licence)

- Jumatatu hadi Ijumaa - Saa 6.00 mchana hadi saa 5.usiku.
- Jumamosi, Jumapili na siku za Sikukuu - Saa 5.00 asubuhi hadi saa 5.00 usiku.

- Mfanyabiashara yeyote wa pombe anapaswa kufuata utaratibu huu ambao ni wa kisheria.

MAKOSA

Baadhi ya makosa chini ya sheria hii:

i. Kuruhusu biashara nyingine isiyokubalika kisheria kufanyika eneo la biashara.

ii. Kuuza pombe kwa mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na sita (16).

iii. Kuajiri mtu aliye na umri chini ya miaka kumi na sita (16) kuuza pombe.

iv. Kuruhusu mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na sita (16) kukaa eneo la kuuzia pombe.

v. Kutoweka Leseni sehemu ya wazi ambpo itaonekena kwa urahisi na wakaguzi.

vi. Kuruhusu /kuleta fujo katika eneo la biashara.

vii. Kuruhusu eneo la biashara kutumika kama danguro.

viii. Kuuza pombe muda ambao ni kinyume cha sheria.

ix. Kufanya biashara ya kuuza pombe kwa kutumia leseni ya vileo ambayo haistahili.

ADHABU

Mfanyabiashara yeyote anayetenda mojawapo ya makosa haya akikamatwa, atafikishwa mahakamani na akitiwa hatiani atalipa faini au kifungo au adhabu zote kwa pamoja.

USHURU WA MALAZI (HOTEL LEVY)

UTARATIBU WA USHURU WA MALAZI (HOTEL LEVY) CHINI YA SHERIA NA 23 YA 1972

MASHARTI YA KULIPIA USHURU WA MALAZI (HOTEL LEVY)

1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anapaswa kutunza kitabu cha wageni kinachoonyesha wageni waliopanga na kulala kwenye nyumba yake kikionyesha jina la mpangaji,anwani, namba ya simu na taarifa zote muhimu zinazohusika.

2) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni (Guest house) anapaswa kulipa kodi ya asilimia kumi (10%) ya malipo ya nyumba (Guest house charges) kwa mwezi husika. Wamiliki wote wenye mauzo yanayotozwa kodi zaidi ya Tshs. milioni arobaini (40,000,000) kwa mwaka hawatalipa kodi ya malazi bali watalipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

3) Kodi iliyowekwa italipwa kuanzia tarehe moja hadi tarehe saba ya mwezi unaofuata.

UTARATIBU WA KULIPIA USHRU WA MALAZI (HOTEL LEVY)

i. Malipo ya ushuru wa malazi ni lazima yaambatanishwe na fomu ya mapato ya kila siku au kitabu cha wageni na fomu ya mapato ya kila mwezi.

ii. Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atawasilisha fomu ya mapato ya kila siku au kitabu cha wageni pamoja na fomu ya mapato ya kila mwezi ambayo amekwisha jaza. Afisa anayekadiria atapitia kuhakiki kama ni sawa na kuhakikisha mmiliki amefikia vizuri asilimia ya mapato ya malazi ya mwezi.

iii. Mmiliki akishindwa kulipa ushuru kwa muda uliopangwa , siku saba (7) baada ya mwezi husika kumalizika atalipa nyongeza ya asilimia ishirini na tano (25%) ya ushuru unaotakiwa kulipwa, na endapo atendelea kutokulipa, adhabu (penalty) itakuwa inaongezeka kwa asilimia kumi (10%) ya ushuru uliotakiwa kulipwa kila baada ya siku thelethini (30) kumalizika.

MAKOSA

i. Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni kushindwa kulipa ushuruwa malazi kwa muda unaotakiwa.
ii. Kushindwa au kukataa kuwasilisha fomu au kitabu cha wageni kila mwezi.
iii. Kushindwa kuweka kitabu na kutunza kitabu chenye kumbukumbu sahihi za wageni.
iv. Kushindwa kutoa risiti, hati za madai na kumbukumbu nyinginezo kama Sheria inavyotaka.
v. Kumzuia Mkurugenzi au Mwakilishi wa Mkurugenzi katika kufanya kazi zake zilizowekwa na Sheria au Kanuni za Ushuru wa malazi.
vi. Kushindwa kutakeleza Ilani iliyotolewa na Kamishna/Mkurugenzi ya kuitwa na kuwasilisha nyaraka zainazohusu nyumba yake ya kulala wageni.
vii. Kutoa taarifa ya uongo kwenye kumbukumbu yoyote inayotumika kwa ajili ya kudanganya au kushindwa au kukataa kujibu maswali vizuri kwa Afisa wa Serikali aliyepewa madaraka na sheria hii.

ADHABU

i. Mmiliki atakayetenda mojawapo ya makosa yaliyotajwa hapo juu atalipa faini isiyopungua Tshs. elfu hamsini (50,000/=) kwa Mkurugenzi wa Halmashauri na isiyozidi Tshs. laki tano (500,000/=) Mahakamani akipatikna na hatia.

ii. Mmiliki anayekwepa kulipa ushuru wa malazi kwa makusudi akikamatwa na kutiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Tshs. milioni mbili (2,000,000/=).